

YAKINI



Hilo si linawafanyia tu jambo fulani? Hakika linafanya. Hebu na tuinaame sasa katika maombi.

² Bwana, jinsi ambavyo imeelezwa kwetu katika wimbo huu wa kupendeza wa kidini, *Jinsi Wewe Uliuyo Mkuu*, nasi tunawazia, asubuhi ya leo, tungefanya nini kama haikuwa ni kwa sababu Yako! Halafu basi tunapowazia kwamba Wewe ni mkuu sana, na kisha upendo Wako ulikulazimisha Wewe kutujali sana, basi ni vigumu kwa nafsi yangu kupokea hilo. Ni kweli. Ninaomba ya kwamba Wewe utatubariki leo, sasa tunapozidi kuingia katika ibada, kwamba Wewe utatumegea Mkate wa Uzima, ambao ni ufunuo wa Kristo. Kwa kuwa tunaomba hayo katika Jina la Yesu. Amina.

³ Ndugu Ungren huja maskanini kila mara. Naye anaishi Memphis, Tennessee, yeye na mama yake, mke wake. Na familia yote huja kwenye maskani. Na ni nadra sana ninapata kumsikia, kwa sababu daima kuna shughuli nyingi, lakini asubuhi ya leo nilikusudia kumsikia akiimba wimbo huu. Yeye huimba mwingine, mmoja wa zile ninazopenda sana, *Kushuka Kutoka Utukufuni Mwake*. Nazo ni nyimbo ninazozipenda sana. Na nilikuwa na majaliwa makuu ya kukutana na baba yake, asubuhi ya leo, mara ya kwanza ambapo nimewahi kuwa na majaliwa hayo, mtu mwema. Ba—basi Ndugu Ungren, baba yake, ha—hataondoka mradi mwana wake anaishi, Morris, kwa sababu kwa kweli wanafanana.

⁴ Naye mke wake, mama yake Ndugu Morris Ungren, ameishi tu miaka hii kumi na mitano iliyopita kwa neema ya Mungu. Kwa hakika yeye amekuwa ni uvuvio mkuu kwangu mimi, kuona hilo; kupitia saa za giza ambazo amepitia, na hata hivyo angali anashikilia mkono wa Mungu usiobadilika. Hutudhihirishia uhalisi wa Ukristo, na imani ya wale wanaoiamini. Kwa hiyo, nina furaha sana kwa hilo asubuhi ya leo.

⁵ Ndiyo kwanza tuwe na arusi, kwenye orofa ya chini. Wawili wa watoto wangu wameoana, na watoto wangu kutoka maskanini; maskini Billy Simpson wetu na maskini msichana wa Myers, wamekuwa wapenzi kwa muda; Sharol, naam. Walikuwa . . . Wao pia ni jamaa hapa, ama maskini Sharol Myers ni jamaa, wa Ndugu Ungren na hao. Kwa hiyo, tuna furaha kwa ajili yao, ninaona wamechukua mahali pao, baada ya kuoana, wamerudi moja kwa moja kwenye ukumbi wa kanisa, na kuketi chini kuisikiliza ibada. Watoto hao daima wamekuwa na mahali katika kilindi cha moyo wangu, kwa sababu wana heshima sana kwa Neno. Wa—wanalipenda tu Neno. Sidhanii kwamba, kwamba ninawaita watoto wangu, sidhani kwamba wao ni bora

kuliko watoto wengine. Bali wanaonekana tu kwangu, nami ni—ni—ninamtazamia Mungu kwa ajili yao.

⁶ Maskini Billy alitaka kuoa, na ndipo alihofia alikuwa anaenda kujiunga na jeshi. Na kulikuwa na wawili ama watatu wao katika hali iyo hiyo. Basi wavulana hao wakanijia, na kusema, “Ndugu Branham, sisi—sisi hatutaki kuwa wazembe au chochote, bali tungetaka wewe umwombe Mungu.” Nao wakanipa msingi wa wao kutaka kutojiunga na jeshi, kama wangeweza; si kwa sababu hawakutaka kuitetea nchi, kwa chochote ambacho wangeweza kufanya. Lakini jambo lilikuwa, kwamba kama wange—kama wangeenda, walikuwa wanaenda kuingia miongoni mwa watu wabaya huko nje katika hayo (sijui mnayaitaje) maPX, ama chochote mnachoyaita, halafu wanaenda huko nje ambapo hao wanawake nusu uchi wanafanya yasiyofaa. Hapo si mahali pa mvulana Mkristo, na kwa hiyo Mungu akawajalia haja yao.

⁷ Na sasa maskini Billy anakuja asubuhi ya leo, kuunganishwa katika ndoa na maskini huyu Sharol anayependeza, kwa hiyo tunawafurahia. Nasi tunawatakia heri katika Ufalme wa Mungu, kwa ajili yao.

⁸ Na sasa huu umekuwa ni wakati mkuu kwetu. Tunalo darasa la kupendeza sana la Shule ya Jumapili hapa asubuhi ya leo, kanisa lililojaa, kwa hiyo tuna furaha sana. Basi mara nyingi, wahudumu, i—inatutia moyo kuona watu wakija na kukusikiza. Maana, unaona, hupendi kuzungumzia viti vitupu, kwa sababu wao... Tungezungumza vile vile tu kama kuna mtu mmoja hapa. Lakini hata hivyo inaleta hisia nzuri unapowazia, “*Huyu* akilikosa, yule mwingine atalipata.” Unaona. Nayo huifanya tofauti, huifanya tukufu.

⁹ Na sasa, katika usaili tu sasa, hii ni, kama tunaweza kuzipitia upesi tu.

¹⁰ Nilikutana na Ndugu Boutliere nilipotoka nje, na sikuwa nimemwona tangu nimekuwa hapa. Nikasema, “Umekuwa wapi?”

Akasema, “Nikiandaa mlo wa batamzinga kwa ajili yao.”

Na kwa hiyo nilikuwa nikimwambia nilikuwa nimepoteza wengine. Akasema, “Wewe?”

Nikasema, “Hujabadilika hata kidogo.”

Akasema, “Wala hata wewe.”

¹¹ Nikasema, “Hiyo ni diplomasia kwelikweli.” Nikasema, “Lakini, unajua, nimebadilika. Nimetoka kwenye mia moja na sabini, hadi kwa mia moja na arobaini na tano, kwa hiyo hakika nimebadilika.” Suti zangu zote, pia, kidogo ni kubwa kupita kiasi kwangu. Na mtu fulani ndiyo kwanza aninunulie moja hivi majuzi, kwa hiyo naweza kuivaa hapa chini; moja ambayo halikupwaya kwenye mabega, na sehemu ya kiunoni kupita.

¹² Bali nina—ninajaribu kufanya vizuri kabisa niwezavyo kwa ajili ya Yesu Kristo wakati nikiwa na fursa ya kufanya hivyo. Na kuhudhuria kwenu kuzuri!

¹³ Nilikuwa nikisimulia chumbani sasa hivi, nilimwona Roho Mtakatifu mkuu akiondoa kansa kutoka kwa mwili wa mwanamke fulani, mumo humo ndani. Yeye ni—yeye ni mwanamke kutoka Texas. Na mama fulani ameketi pale, ambaye sijamwona mtu mwenye fadhaa, mke wa mhudumu, dakika chache tu zilizopita. Ndipo Bwana akanionyesha ono lake akiwa ameketi pale, nami nikamwona. Alipitia New York, naye alitaka kupenya hapa juu. Alikuwa tu na dakika tano pekee, ndipo nikamwona mumewe akiugua vidonda vya tumbo, na kilichosababisha vidonda hivyo kilikuwa ni kujali kwake mke wake. Mungu Mwenyezi, mtulize mwanamke huyo anayeketi pale. Ameketi, akiniangalia sasa. Kwa hiyo, na pia ninataka kukuambia, ndugu, kidonda chako cha tumbo kimekwisha. Unaona? Naam, unaenda kuwa mzima sasa na kurudi kwenye kazi ya Bwana.

¹⁴ Sasa, ukiona jambo ambalo Bwana anatenda, hu—huwezi tu kutosheka juu ya hilo. Unataka tu kuendelea, kuendelea, kuendelea, kuendelea.

¹⁵ Na, sasa, jana usiku tulikuwa na ibada nzuri ya maombi, na hilo ni jema, hilo ni sawa. Kuweka mikono juu ya wagonjwa, hilo ni jambo jema. Hayo ndiyo yote yanayohitajika, wakati mwingine. Halafu basi kuna wengine ambao kuna kitu fulani huko nyuma, ambacho wao—wao hawawezi kukishika, na inakubidi kumpata mtu huyo na kuchunguza kuona kuwa hicho ni nini. Unaona, kuna kitu ambacho kinawazuia, kitu kinachokaa njiani. Na kivuli kimoja kidogo kitakitetemesha na kukiondolea mbali.

¹⁶ Sasa, maskini yule mama mle ndani dakika chache zilizopita, alikuwa na wasiwasi mwingi, amefadhaishwa mno. Maskini jamaa mdogo, hata asingeweza kupumua. Alikuwa tu... [Ndugu Branham anavuta na kutoa pumzi, akihema ili kupata pumzi—Mh.] na ku—kufanya tu yasiyofaa, unaona.

¹⁷ Sasa, jambo linalokubidi kufanya. Hii hapa undani tu kidogo, unaona. Ni kushika roho yake. Unaona? Ndipo basi unavurumisha kwake wazo lako lenyewe. Unaona? Halafu unabadilisha kuwaza kwako. Unaona? Ndipo wakati ikifanya hivyo, basi unaweza kumwekea msingi juu ya Kristo, na kuanzia hapo anaweza kuendelea. Lakini inakubidi kubadilisha njia yake ya kuwazia, unaona. Hawezi kuibadilisha mwenyewe. Anakimbia tu katika mzunguko mkali, na inakubidi kushika hiyo. Sasa kuna kitu fulani kidogo kinachokupa ninii... Usijaribu kuichunguza; usifanye hivyo. Amini tu na uendelea.

¹⁸ Mtoto yule mchanga angewezaje, akiwa amelazwa katika mikono ya mama yake, alikuwa amefariki tangu saa tatu asubuhi

hiyo, na usiku sana usiku huo, maskini roho hiyo ilikuwa wapi? Inakubidi kuenda kuitafuta roho hiyo na kuirudisha. Na ndipo wakati ukiiona ikirudi, basi unaweza kusimama katika Jina la Bwana na kuiita. Unaona, basi itatendeka. Lakini hadi ufanye hivyo, unapoteza tu pumzi lako, unaona.

¹⁹ Si kitu—kitu cha ajabu sana. Ni kumpata Mungu, hata kujiondoa mwenyewe njiani na kumruhusu Roho Mtakatifu akutumie kwa chochote Yeye anachotaka kufanya. Jambo ndilo hilo. Jambo muhimu, kwa karama yoyote, ni kuondolea mbali mawazo yako mwenyewe, na kumruhusu Kristo. Halafu chochote Hilo lililosema, kama ukitaka kujua kama ni Kristo au sivyo... Msisimko tu, achana nao. Lakini kama ni mhemko tu, achana na huo. Lakini kama imeandikwa katika Neno, basi ni Mungu. Daima amua kila kitu, ambacho roho yoyote inakuambia, kwa Neno. Neno, kamwe usiliondokee hilo Neno; ukiliondokea, umepotea.

²⁰ Sasa, kabla hatujakaa mpaka wakati wa adhuhuri, tukizungumza tu namna hiyo, hebu tugeuke tu kwenye Biblia na kusoma baadhi ya Maandiko hapa. Ndipo basi tunaenda ku... Ninapenda Neno la Mungu. Ninajua sote tunalipenda. Sasa haikuwa na...

²¹ Nilikuwa ninaenda kuhubiri, asubuhi ya leo, au kuzungumza, kufundisha shule ya Jumapili, juu ya siri za Mungu zilizofichika tangu msingi wa ulimwengu, kufunuliwa ndani ya Yesu Kristo. Na sikuipata nafasi ya kuyapitia yote. Nilisahau kuhusu arusi inayokuja, kwa hiyo hu—huenda nikafikia hiyo wakati mwingine unaokuja.

²² Sasa ninaenda kusoma baadhi kutoka sehemu tatu katika Biblia. Ya kwanza, ninataka kusoma kutoka katika Wafilipi 1. Mlango wa kwanza wa Wafilipi, nikianza na kifungu cha 19, na kusoma pia hadi cha 22.

Maana najua ya kuwa haya yatanigeukia kuwa wokovu wangu, kwa sababu ya kuomba kwenu, na kuruzukiwa Roho wa Yesu Kristo;

Kama vile nilivyotazamia sana, na kutumaini, kwamba sitaajibika kamwe, bali kwa uthabiti wote, kama sikuzote, na sasa vivyo hivyo Kristo ataadhimishwa katika mwili wangu; ikiwa kwa uzima, au kwa mauti.

Kwa maana kwangu mimi kuishi ni Kristo, na kufa ni faida.

Ila ikiwa kuishi katika mwili, kwangu mimi ni matunda ya kazi; basi... nitakalolichagua silitambui.

²³ Sasa katika Kitabu cha Warumi. Na tunataka kuanzia kwenye mlango wa 8 wa Warumi, na kifungu cha 35, kujenga juu ya kile ninachotaka kuchukua kama fungu.

Ni nani atakayetutenga na upendo wa Kristo? Je! ni dhiki au shida, . . . adha, . . . njaa, au uchi, . . . hatari, . . . upanga?

Kama ilivyoandikwa ya kwamba, Kwa ajili yangu tunauawa . . . mchana kutwa, tumehesabiwa kuwa kama kondoo wa kuchinjwa.

Lakini katika mambo hayo yote tunashinda, na zaidi ya kushinda, kwa yeye aliyetupenda.

Kwa maana nimekwisha kujua hakika ya kwamba, wala mauti, wala uzima, wala malaika, wala wenye mamlaka, wala nguvu, wala yaliyopo, wala yatakayokuwapo, wala . . .

Wala yaliyo juu, . . . yaliyo chini, wala kiumbe kinginecho chote, hakitaweza kututenga na upendo wa Mungu ulio katika Kristo Yesu Bwana wetu.

24 Katika Matendo 2, na kifungu cha 30.

Basi kwa kuwa ni nabii, akijua ya kuwa Mungu amemwapia kwa kiapo, ya kwamba katika uzao wa viuno vyake kulingana na mwili atamketisha mmoja katika kiti chake cha enzi;

25 Sasa haya ni Maandiko mengi, kwa namna fulani kuzunguka kutoka mahali pamoja hadi pengine, katika Biblia. Lakini tunajua kwamba, kama kiasi hiki cha Maandiko kimesomwa, tunaenda kupata kitu Humo ndani ambacho kinaenda ku—kutusaidia. Sasa hebu Mungu na atusaidie sasa, kwa vile ningetaka kuchukua somo hili, asubuhi ya leo, kama neno la yakini: *Yakini*.

26 Sasa sisi, nilipokuwa nikiangalia fungu hili, nilienda kwenye kamusi. Nikawazia, “Nini? Mtu fulani anaendelea kusema, ‘Hiyo ni yakini, kweli. Yakini, ndilo hili.’” Nikawaza, “Neno hilo ni nini? Linamaanisha nini, *yakini*?” Ndipo nikaenda kwenye kamusi kuona kile linachomaanisha.

27 Webster inasema ni “kamilifu lenyewe, halina mipaka katika nguvu zake, kimsingi ni mkataa.” Unaona, “halina ukomo katika nguvu zake, kamilifu lenyewe, na kwa kweli ni mkataa,” neno *yakini*.

28 Nami ningependa kusema hili, na ninatumaini kwamba mtayashika maneno haya, maana mimi si kasisi aliyefunzwa katika jinsi, na njia ya kisaikolojia ya kuleta kitu fulani cha kuvutia ambacho kingewashikilia watu. Jambo la pekee ninalofanya, ni kujaribu kufanya vizuri niwezavyo, kwa sababu ya marafiki ambao Kristo amenipa, nami ni—ni—ninawataka waone kilicho wazo langu kuhusu Kristo.

29 Sasa, kila fanikio kubwa limefungamana na yakini. Huwezi kuendesha maisha bila kuwa na yakini. Huwezi kuwa na mafanikio bila ya kuwa ni yakini, kwa kuwa ndiyo nguzo ya

mwisho. Ni—ni shubaka la mizigo kwenye mwisho wa safari. Ni mahali ambapo umefungiwa kwenye kitu fulani.

³⁰ Katika siku tunayoishi sasa, na kila kitu kinavunjika sana, ni dhaifu sana na kujisahau, nafikiri ya kwamba Ujumbe huu ungekuwa ni kitu kinachofaa sana, hasa kwa Wakristo wakati wanapopitia matatizo yao ya kilindi sasa. Kanisa la Kikristo linapitia matatizo makubwa liliyopata kuwa nayo kwa miaka elfu mbili iliyopita. Kwa sababu, tunafikia mahali ambapo pana kitu kimekabidhiwa Ukristo, kitu ambacho hawana budi kufanya uamuzi juu yake, nami nafikiri kwamba kanisa la Kikristo linapaswa kuwa na kitu fulani ambacho wanajua kwamba wamefungiwa, badala ya kuelea tu kama jani juu ya maji, upepo. Kama Biblia ilivyosema, “Wakichukuliwa na kila upepo wa mafundisho.” Upepo huja na kupeperusha jani hilo dogo upande *huu*, na kisha upepo mwingine unakuja, upepo wa kaskazini, upepo wa kusini, upepo wa mashariki, upepo wa magharibi. Hutafika popote, hujaimarishwa. Maisha ya Mkristo yanapaswa kuwa ni maisha yaliyoimarishwa. Yanapaswa kuwa ni kitu fulani ambacho—ambacho ni kanuni ambayo—ambayo umefungiwa, ambayo ni zaidi ya maisha yenyewe.

³¹ Basi lazima uwe na kitu fulani ulichofungwa kwacho. Baadhi ya watu wamefungiwa kwenye biashara yao. Wengine wamefungiwa kwenye familia zao. Wengine wamefungiwa kwenye kanuni ya imani. Wengine wamefungwa kwa nguzo ya jeshi. Tuna mambo mbalimbali ambayo tumefungwa kwayo. Bali nafikiri, kama Mkristo, tunapaswa kufungwa mahali tunajua ni sahihi, unaona. Kwa sababu, huenda ukafungiwa kwenye familia yako, na mke wa—wako angeweza kukuacha. Unaweza kufungwa kwenye jeshi, na huenda ukauwa. Pia unaweza kufungwa kwenye vitu vyovyote mbalimbali, nacho kina mwisho. Lakini lazima kuwe na nguzo ya mwisho ya kufungiwa. Hapana budi pawe na mahali ambapo—ambapo mtu inambidi kufungiwa kwa ajili ya hatima yake ya Milele. Kwa sababu, kama utatumaini katika kazi yako, kazi yako ikiisha, imekwisha. Familia yako ikichukuliwa, imekwisha.

³² Lakini kuna kitu kimoja tu ambacho nafikiri ndicho nguzo ya mwisho ya kufungia. Nami ninaamini kwamba Paulo alikuwa na nguzo ya kufungiwa maishani mwake hapa. Na ningependa ku—kuunga mkono, kama tungekuita hivyo, na kuzungumzia nguzo hiyo ya kufungiwa. Alisema, “Kwangu mimi kuishi ni Kristo, na kufa ni faida.” Sasa, Kristo alikuwa ndiye Yakini ya Paulo. Ilikuwa ni nguzo yake ya kufungiwa. Ilikuwa ni yake. Ilikuwa ndiyo mwisho wa mabishano yote. Ilikuwa ni Kristo, alikuwa ndiye nguzo yake ya kufungiwa.

³³ Paulo hakuwa na nguzo hiyo ya kufungiwa siku zote. Alikuwa anafungwa kwenye kundi la Mafarisayo. Na ilimbidi kufunzwa na kuelimishwa, ili kwamba waweze kumkubali na kumruhusu ajifunge mwenyewe kwenye nguzo yao. Bali siku

moja alikuwa njiani kuelekea Dameski, ndipo akakutana na Yesu, uso kwa uso. Na kuanzia hapo alijiweka huru kutoka kwa nguzo yake ya kufungiwa ya Kifarisaayo; na kujifunga tena, kwamba Yesu Ambaye alijua alisulubiwa, akafa, na kufufuka tena. Paulo alijua hayo kwa sababu alikutana na Mtu huyo. Hiyo ilimbadiisha papo hapo. Hakuwa yule yule tangu hapo na kuendelea. Hakukutana tu na kitabu. Hakukutana tu na ka—kanuni ya imani. Alikutana na Mtu, Yesu Kristo. “U nani Wewe, Bwana?”

Akasema, “Mimi ni Yesu.”

³⁴ Hebu tuwazie wongofu huo, kwa dakika chache. Ninaamini Paulo alikuwa mtu mwaminifu. Kwa kuwa hii ni shule ya Jumapili, tunataka kuifundisha kama shule ya Jumapili. Paulo, ninaamini, alikuwa mtu mwaminifu, sana, na kulikuwa—hakukuwa na chochote kumhusu kilichokuwa tofauti na mtu yeyote mwingine.

³⁵ Manabii hao wote walikuwa tu watu kama tulivyo sisi. Biblia ilisema hivyo. Mtakatifu Yakobo 5, “Eliya alikuwa ni mwanadamu mwenye tabia moja na sisi,” alikuwa na mema na mabaya yake, kuingia na kutoka kwake, “na aliomba kwa bidii ili kusinyeshe mvua.”

³⁶ Naye Paulo alikuwa ni mwanadamu kama tulivyo sisi. Alikuwa na mahangaiko yake, shaka lake. Naye alikuwa ni mtu mwaminifu. Alikuwa anahudhuria moja ya kundi zuri sana la kidini lililokuwepo ulimwenguni. Naye alikuwa anakuwa mwalimu wa kundi hilo; aliyefunzwa chini ya mwalimu mashuhuri, Gamalieli, ambaye alikuwa ni mmoja wa walimu mashuhuri kuliko wote waliokuwa nao wa siku hiyo. Wazazi wake walilishughulikia, waliona kwamba kulikuwa na kitu katika maisha ya Paulo, na wakafanya kazi kwa bidii kumpeleka shuleni, ili aweze kufunzwa katika amri zote za Mungu. Na, kwa uaminifu wenye kina, aliamini kila neno lake.

³⁷ Pia alikuwa amesikia kuhusu tabaka hili duni la watu, na jinsi ambavyo kulikuwa na nabii, alivyodhaniwa, na kundi Lake, aliyekuwa ameinuka katika Galilaya, aliyedhaniwa kutenda miujiza na kuwaponya wagonjwa. Lakini ninii yake—kundi lake alilokuwa mshirika wake lisingeweza kumkubali Mtu huyu kuwa ni nabii, huyu Yesu wa Nazareti, kwa sababu Yeye hakuwa amejitambulisha Mwenyewe pamoja nao. Kwa hiyo Paulo asingaliweza kuendea hilo, kwa sababu kundi lake mwenyewe la—la watu hawakuliamini Hilo. Nao walikuwa wamemwonya dhidi ya kama hayo.

³⁸ Basi Paulo, akiwa mwaminifu, aliwazia, “Ikiwa kitu hiki si cha Mungu, na kanisa langu linasema kuwa si cha Mungu, basi lipo jambo moja tu la kufanya, ni kukiondolea mbali.” Kasema, “Kiondoe njiani, kwa sababu ni...kingekuwa ni kizuizi, kingekuwa ni kivimbe, donda ndugu,” dhidi ya dhehebu

lake la imani. Kwa hiyo akakusudia moyoni mwake kwamba angeondoka kwenda na kulikatilia mbali hili “donda ndugu,” kama alivyoliita, ama kanisa lake lilivyoliita, kutoka kwenye kundi lake zuri la Kifarisayo.

³⁹ Siku moja, akiwa na nyaraka mfukoni mwake, kutoka kwa kuhani mkuu, kuwatia mbaroni hao watu wote waliokuwa katika hali hiyo, kwa sababu hilo ndilo jukumu ambalo Paulo alikuwa nalo. Alikuwa njiani mwake kuelekea kwenye mji uitwao Dameski. Walikuwa wamewanyamazisha, kote katika Yerusalemu. Kwa hiyo alikuwa—alikuwa amempiga mawe Stefano, naye Paulo alimfanya kupigwa mawe, alitoa ushahidi na kushikilia koti. Sasa angeenda huku chini na kufanya jambo lile lile, na kuondolea mbali kizuizi hiki kikubwa.

⁴⁰ Lakini yapata, lazima ilikuwa ni yapata wakati wa adhuhuri, karibu saa tano, saa sita, aliangushwa chini. Na wakati alipoangushwa, alitazama juu na hapo palikuwa na Nuru iliyosimama mbele yake. Nayo Sauti ikitoka kwenye Nuru hii, ikisema, “Sauli, Sauli,” swali, “mbona unanitesa Mimi?” Sasa Paulo alijua, ama Sauli, hasa, alijua kwamba watu wake walikuwa wakiifuata Nuru iyo hiyo tangu walipotoka Misri. Basi ikiwa . . .

⁴¹ Hivi mliwahi kuona tafsiri ya Lamsa ya Biblia, ninii ya kale . . . A—alama ya kale ya Kiebrania ya—ya Mungu ni Nuru pmbetatu; takriban, kitu kama *hicho*, kwamba sifa tatu za Mungu, ndani ya Uungu mmoja. Basi Nuru hii pmbetatu, hizo tatu ndani ya Mmoja, kuwa ni Mungu mmoja, ilikuwa ni i—ishara kwa Mwebrania, ya Mungu, Nuru.

⁴² Halafu basi wakati Musa alipokutana na Yeye kwenye kichaka, ndipo Yeye akasema, “MIMI NIKO,” ambayo inabaki vile vile, tatu; jana, leo, na hata milele, bado ni Mungu yeye yule. Na Musa alikutana na Yeye katika kichaka kilichowaka moto. Yeye alikuwa ni Nuru. Basi wakati Yeye alipowaongoza wana wa Israeli kutoka nyikani, Yeye alikuwa ni yule Malaika wa agano, ambaye Musa kwa imani aliona, akaiacha Misri, akihesabu shutuma la Kristo kuwa ni hazina kubwa kuliko ile ya Misri. Kwa imani, Musa aliona kwamba huyo alikuwa ni Kristo, ule Upako. Nao Upako ulikuwa hauko juu ya mtu maalumu, bali Huo ulikuwa katika umbo la Nguzo ya Moto. Unaona?

⁴³ Ndipo basi Upako uo huo ukashuka kwenye ubatizo Wake, na kuingia ndani ya Kristo na kukaa ndani Yake. Yohana alijua ilikuwa ni Yeye. Alisema, “Yule Ambaye juu yake utamwona Roho aliyewaongoza kutoka Misri kuingia nyikani, na kutoka nyikani kuingia katika nchi ya ahadi, Yule ambaye utalionaye hili pmbetatu la Mungu likishuka na kukaa juu yake, Huyo ndiye Ambaye atabatiza kwa Roho Mtakatifu na Moto.”

⁴⁴ Sasa Paulo hakuwa amejaliwa kuona hili bado. Lakini ili tu kulifanya kuwa kweli, kwako, Wayahudi walikatazwa kabisa

kuinama mbele ya sanamu, ama chochote namna hiyo! Sasa wakati alipoiona Nuru hii kuu, alijua kwamba huyo alikuwa ni Bwana. *Bwana* linamaanisha “umilikaji, udhibiti wa.” A—asingeliita tu kitu chochote kile “Bwana,” huyo Mwebrania mwaminifu, wakati alijua kwamba Huyu alikuwa ni Roho. Bali tazama, alijua kwamba Nguzo iyo hiyo ya Moto ilikuwa Ndiyo ambayo ilikuwa imewaongoza watu wake. Ndipo basi anarudi na kasema, “Bwana, U nani Wewe? U nani Wewe? Ninataka kujua Wewe ni Nani? Ulikutana na Musa katika jina la ‘MIMI NIKO.’” Lakini nitakomea hapo na wazo lao, kwa dakika moja.

⁴⁵ Yesu, wakati alipokuwa duniani, ametiwa upako na Huo waliouona, tazama, Yeye alisema, “Nimetoka kwa Mungu,” Roho, ile Nuru, ile Nguzo ya Moto, “tena ninarudi kwa Mungu.” Basi alifanyika mwili kusudi aweze kufa kwa ajili ya dhambi zetu. Ndipo baada ya kifo Chake, kuzikwa, kufufuka, na kupaa juu, baada ya Yeye kupaa juu; kwenye siku arobaini, Yeye alipaa juu; na kwenye siku ya hamsini, Yeye alirudi katika umbo la Nguzo ya Moto, miongoni mwa watu, na kujigawa Mwenyewe, kama ndimi za moto, na kutulia juu ya kila mmoja wao. Na ndipo wote wakajazwa na Roho Mtakatifu, na kuanza kuzungumza kwa lugha zingine, kama Roho alivyowajalia kunena.

⁴⁶ Mnaona, Mungu akijigawa Mwenyewe; Mungu kwanza katika Nguzo kuu ya Moto; Mungu akidhihirishwa katika mwili wa mwanadamu; sasa Mungu akijigawa Mwenyewe miongoni mwa watu Wake. Nguzo ya Moto ikipasuka, na kukaa juu ya kila mmoja wao, kama ndimi za moto zilizogawanyika, ndimi zilizogawanyika zilikaa juu yao, ndimi za moto, ndimi zilizogawanyika kama moto zilikaa juu ya kila mmoja wao. Na wote wakajazwa na Hiyo, na wakaanza kunena kwa lugha, kama Roho alivyowajalia kunena.

⁴⁷ Sasa, mnaona, sisi si watu waliogawanyika, inatubidi kuwa katika umoja, kwa sababu kila mmoja wetu anabeba sehemu ya Mungu. Basi lazima tuje pamoja, na halafu Nguzo ya Moto inadhihirishwa katika utimilifu, katika ukamilifu Wake; wakati Kanisa Lake linapoketi pamoja katika mahali pa Mbinguni, ndipo utimilifu wa nguvu za Mungu zimo ndani ya Kanisa Lake. Kila mmoja wetu akishikilia karama za kiroho na ofisi za kiroho, tukija pamoja, kunarudisha hiyo Nguzo ya Moto tena.

⁴⁸ Naye Paulo alitambua hiyo kuwa ni ya Bwana, ndipo akasema, “Bwana, U nani Wewe, kama ninakutesa Wewe?”

⁴⁹ Yeye akasema, “Mimi ni Yesu, na ni vigumu kwako kupiga teke michokoo.”

⁵⁰ Basi Paulo akaamriwa kuamka na kuenda chini katika barabara inayoitwa, “Nyofu.” Na hapo palikuwapo nabii aliyesimama, jina lake Anania, na akaona ono, na kumbatiza. Basi akashuka akaenda chini huko Arabia, kwa miaka mitatu,

kuchunguza Maandiko, kuona kuwa hii Nguzo ya Moto iliyoonekana kwake ilihusu nini.

⁵¹ Sasa tunaona kwamba Paulo, maisha yake yote, alikuwa na hiyo kama nguzo yake ya kufungiwa. Alikuwa amekutana na Mungu, uso kwa uso, na aliagizwa na Mungu. Ni nguzo ya jinsi gani! Ni Yakini ya jinsi gani! Huo ulikuwa ndio mwisho wa mabishano yote. Huo ulikuwa ni mwisho wa kila kitu kwa Paulo. Ugomvi wote, kila kitu kilitoweka. Sijali kile Mafarisayo walichosema, Masadukayo walichosema, au mtu yeyote mwingine; alikutana na Mungu aliyethibitishwa na Neno, hilo lilitosha! Hayo yalikuwa ndiyo maisha yake yote tangu hapo. Kwa kuwa alikuwa amemwona Mungu akidhihirishwa, na ilikuwa imethibitishwa kwake kwamba Huyu alikuwa ni Mungu, kwa Neno, na kwa umbo na sura aliyokuwa ndani yake, na kwa Sauti iliyosikika iliyonena naye hasa kile ilichokuwa. Sasa, hilo lilikuwa ni jambo kuu. Si ajabu angeweza kusema, mbele ya—ya Agrippa, “Sikuliasi lile ono la Mbinguni.” Alifungwa kwalo. Kulikuwa na kitu halisi, kitu alichokijua, kitu ambacho hakuna mtu angaliweza kukiondoa kwake.

⁵² Sasa, leo, ikiwa tunategemea tu elimu, ama nji—njia ya kimitambo ya—ya elimu kuelezea Biblia, basi tumeipata tu kutokana na dha—dhana ya kiakili. Lakini hakuna mtu aliye na haki nyuma ya mimbara hii, kuhubiri Injili, isipokuwa amekutana uso kwa uso na Hiyo.

⁵³ Kama vile Musa, upande wa nyuma ya jangwa, haijalishi jinsi alivyoelimika vizuri, chochote kilichokuwa kimetendeka; hofu zake na fadhaa ziliondoka kwa sababu alisimama mahali patakatifu pamoja na Mungu, ambapo hapana mtu angaliweza kuliondoa kwake.

⁵⁴ Na kila mwanamume au mwanamke aliye na uzoefu na Mungu, amekutana na Nguzo ii hii ya Moto juu ya mahali patakatifu pa moyo wako. “Hakuna mwanatheolojia, hakuna ibilisi, hakuna chochote,” Paulo alisema, “hakuna kitu kilichopo, hakuna kitu kitakachokuwapo, mauti, ugonjwa, huzuni, kiwezacho kututenga na upendo huo wa Mungu, ulio katika Kristo Yesu.” Ni mhimili wa kufungiwa. Unajua jambo fulani lilitendeka. Haijalishi ni jinsi gani sayansi inavyoinuka na kusema *hili*, *lile*, au *linginelo*, wewe umefungwa. Wewe na Mungu mnakuwa kitu kimoja. Yeye yuko ndani yako, na wewe ndani Yake. “Katika siku hiyo mtajua ya kwamba mimi ni ndani ya Baba, Baba ndani Yangu; Mimi ndani yenu, nanyi ndani Yangu.” Umefungwa Kwake.

⁵⁵ Basi Paulo alikuwa na ma—maisha yaliyotiwa msingi juu ya Kristo. Yalikuwa ni maisha tofauti na yale aliyokuwa nayo wakati mmoja. Wakati mmoja alikuwa na dhana ya kielimu; lakini sasa anayo maisha yaliyowekwa msingi juu ya Kristo, yakini. Haijalishi ni kiasi gani Agrippa angeweza kusema,

“Wewe, wewe umerukwa akili, Paulo. Umerukwa na akili. Wewe, wewe ulisoma kupita kiasi,”

Akasema, “Sina kichaa.”

⁵⁶ Ndipo basi alimfadhisha sana Agrippa, hivi kwamba yeye alisema, “Wewe karibu unishawishi mimi kuwa Mkristo.”

⁵⁷ Akasema, “Laiti ungalikuwa, isipokuwa tu... kama nilivyo mimi, isipokuwa vifungo hivi.”

⁵⁸ Inakufanya kutenda mambo, ukipata maisha yaliyotiwa msingi juu ya Kristo kama aliyokuwa nayo Paulo, kikawaida usingaliweza kufanya. Sasa angalia. Kikawaida, mtu huyo alifunzwa katika Maandiko yo—yote na kadhalika, kikawaida angalifuata mkondo huo aliofunziwa. Bali wakati alipofanyika... na kumfanya Kristo kuwa yakini yake, mkataa wake, ndipo kukawa na maisha tofauti. Alitenda tofauti. Alfanya mambo kiwazimu, kwa kile ambacho wakati mmoja alifunzwa kufanya. Nayo itafanya jambo lilo hilo.

⁵⁹ Iwapo kanisa lingeondoka kwenye hilo Baraza la Makanisa, na kurudi na kulifanya Neno la Mungu kuwa mkataa kwao, kulifanya Neno la Mungu nguzo yao ya kufungiwa, hilo lingelitekeleza. Bali wanajifungamanisha kwenye ufanisi uliobuniwa na mwanadamu. Nao hauna budi kuanguka. Vema, Biblia ilisema kwamba wangepanya hivyo. Lakini kunaenda kuwepo na Bibi-arusi aliyechaguliwa tangu msingi wa ulimwengu, ambaye atafungamanishwa kwenye mhimili huo wa kufungia.

⁶⁰ Ninaweza kuuona Umilele ukijitokeza, unakuja chini kwenye wakati, tangu Edeni. Ndipo, wakati Huo uliposhuka, kukaja mstari wa Damu, kote hadi kufikia Kalvari; na kutoka Kalvari, ukafungamanishwa na mstari huu, na unaenda hadi kwenye nguzo ya kufungia, Yesu. Basi wakati mmoja atakapokuja kudai walio Wake, kila mtu aliyefungiwa kwenye yakini hiyo atainuliwa kuingia katika Umilele. Kwa nini? Wamekuwa katika Umilele wakati wote. Walichaguliwa kimbele katika Umilele. Wao ni sehemu ya Mungu. Walikuwa katika mawazo Yake hapo mwanzo. Basi kamba hiyo kubwa ikivutwa, ya mstari wa Damu, ile Ishara niliyokuwa nikizungumzia, ikija kutoka ardhini, kila mtu aliyehusishwa katika Damu hiyo atadondoshwa moja kwa moja katika Umilele tena. Lakini njia ya pekee itakayokuwa, itafungiwa kwenye hiyo yakini, Yesu Kristo. Ni yakini! Si mafanikio ya kibinadamu; bali Mungu alimfufua kutoka kwa wafu, na Yeye ni yakini. Nasi tunajua Yeye yu hai, kwa sababu Yeye huyu hapa pamoja nasi katika Nguvu za kufufuka Kwake, akifanya jambo lile lile alilofanya wakati Yeye alipokuwa hapa duniani.

⁶¹ Nimefungwa kwenye hiyo Yakini. Hiyo ndiyo mwisho wa ugomvi wote. Nimefungwa kwayo. Hiyo ni maisha yangu. Nilikuwa mwenye dhambi Kristo aliponiokoa. Nilikutana na

Kitu fulani. Na tangu Hicho kilipoingia ndani yangu, imekuwa—imekuwa tofauti. Nami nimefungwa kwacho, kila kitu nilicho kimefungiwa papo hapo. Na kisha Mungu akigawa maisha Yake, na kuniacha niishi ndani Yake, na Yeye ndani yangu, basi tumefungwa. Mimi. . .

⁶² Haileti tofauti yoyote kile wengine wanataka kuamini. Kwa mtu binafsi, umefungwa kwenye Hicho. [Ndugu Branham anaipigapiga Biblia yake—Mh.] Hicho ndicho mkataa wako. Hicho ndicho. . . hilo ndilo neno la mwisho. Halafu basi kama Yeye ni Neno, basi *Hii* lazima iwe ndiyo neno la mwisho. *Hii* lazima ilitatue. Chochote Hiyo isemacho, Hiyo ndiyo ule ukanda mwekundu. Hiyo ni Kristo. Na chochote kinyume na Hiyo, sijui chochote kukihusu. Hicho ndicho tunachotaka kujua, ni kile Neno hili lisemacho; kwa sababu nimefungwa kwa Kristo, naye Kristo ni Neno. Mnaipata sasa? [Kusanyiko linasema, “Amina.”]

⁶³ Na sehemu ya Neno Lake lilitotengwa kwa ajili ya siku hii, Roho Wake Mtakatifu yupo hapa kudhihirisha sehemu hiyo ya Neno.

⁶⁴ Kama tu ilivyokuwa huko nyuma katika kuzaliwa Kwake. Isaya 9:6. Kote kupitia Maandiko. Kila kitu kilichonenwa kumhusu Yeye, hicho kilitimizwa. Katika Kitabu cha Luka, tunasema ni. . . tunaiona hiyo. Na Yeye alikuwa ndiye mwisho, Yeye alikuwa ndiye—Yeye alikuwa ndiye mwisho wa unabii, pia, kumhusu Yeye. Alitimiza hiyo, historia, nyimbo, kila kitu katika Agano la Kale, kilichozungumza juu Yake, kilitimizwa papo hapo. Hiyo ikawa mkataa. Hiyo ikafanyika nguzo ya kufungia ya Neno la Mungu kwa ajili ya wakati huo.

⁶⁵ Nao watu halisi waliozaliwa mara ya pili wa wakati huu, waliojazwa na Roho Mtakatifu, ni nguzo ya kufungia ya Maandiko haya yanayopaswa kutimizwa katika siku hizi za mwisho. Hayo ndiyo mkataa. Ni mkataa wa Mungu, kwa sababu ni Neno Lake; nalo Neno ni Kristo, nguzo ya kufungia. Hakuna njia ya kuondokea hiyo. Kitu kinachokushikilia.

⁶⁶ Kama nilivyosema, kinakufanya kutenda mambo ambayo kwa kawaida usingeweza kufanya. Kilimfanya Paulo kutenda mambo ambayo asingeweza kufanya kikawaida. Kilimfanya Musa kutenda mambo ambayo asingeweza kufanya kikawaida. Kinamfanya kila mwanaume na mwanamke kutenda mambo ambayo hawangeweza kufanya kikawaida. Ni kitu ambacho ume—umetiwa msingi. Ni kitu fulani, Hicho ni kidhibiti chako. Ni kama ninii. . .

⁶⁷ Ndicho nanga kwa meli. Meli imefungwa kwenye nanga, katika wakati wa dhoruba. Basi ikiwa Kristo ndiye yakini yako, umefungwa Kwake. Katika wakati wa shida, meli, ukiiacha ipepesuke, itapasuka kwenye mi—mi—mi—miamba. Lakini kile wanachofanya, wanateremsha nanga. Nanga hokokoteza mpaka

ishikilie kwenye jiwe la msingi. Ndipo meli inafungiwa kwenye nanga. Ndiyo yakini kwa ajili ya meli.

⁶⁸ Basi Mkristo aliyezaliwa upya amefungwa kwa Kristo, nayo Biblia ndiyo nanga. Ndicho kitu tulichofungiwa. Acha madhehebu, acha kitu tofauti, acha sayansi, acha waelimishaji waseme chochote watakacho. Mradi tu Neno hilo linakisema na kukiahidi, tumefungwa kwenye Hilo. Kuna kitu hakitatuacha tuondoke kwenye hicho. Hiyo ni kweli. Mkristo halisi aliyezaliwa, wanakaa na Neno hilo. Kama Hilo linasema jambo fulani kufanya, na njia ya kulifanya, hivyo ndivyo lazima tulifanye. Haijalishi kile mtu yeyote mwingine asemacho, Hilo ndilo Mungu alilosema. Tumefungwa kwenye Hilo, maisha yaliyotiwa msingi kwa Kristo.

Kristo, tena, ni kama Nyota ya Kaskazini.

⁶⁹ Mnajua, dunia huzunguka. Nazo nyota, hasa, ile unayoiona kama nyota ya jioni, pia ndiyo nyota ya asubuhi. Dunia huzunguka tu kuifikia. Lakini husogea tu mbali na nyota hizo, zote isipokuwa nyota ya kaskazini. Sasa huwezi kuiweka dira yako juu ya nyota ya jioni na uende popote, maana asubuhi itakayofuata, kitu gani? Uko kwenye nyota ya jioni magharibi, na asubuhi inayofuata uko mashariki. Unaona, huwezi kufanya hivyo. Lakini unaweza kuiweka kwenye nyota ya kaskazini, amina, na uiweke katikati kabisa. Utafaulu.

⁷⁰ Na hayo ndiyo maisha yaliyowekewa msingi juu ya Kristo yaliuyo. Ukipotea, Yeye ndiye Nyota yako ya Kaskazini. Basi, kama Yeye ni Nyota ya Kaskazini, Roho Mtakatifu ndiye dira yako, nayo dira itaelekeza tu kwenye Nyota ya Kaskazini. Haitaelekeza kwenye kanuni ya imani wala dhehebu. Haitaelekeza kwenye msisimko, au chochote kile. Itashikilia imara kwenye Nyota ya Kaskazini. Yeye ndiye Nyota yako ya Kaskazini. Ukipotea, huenda ukasogea na madhehebu, na mambo kama hayo. Bali dira, Roho Mtakatifu, atakuelekeza moja kwa moja kwenye Neno, ambalo ni Kristo, na kukushikilia imara. Jifungie kwenye Hilo.

⁷¹ Vipi kama hakukuwepo na nyota ya kaskazini, mtu angeweza kupata njia yake kwenye bahari yenye ukungu? Vipi kama hakukuwa na Roho Mtakatifu kukuelekeza kwenye Neno la Mungu, kudhihirisha Hilo na kulithibitisha, tungefanya nini katika saa hii? Roho Mtakatifu huelekeza tu kwenye Neno. "Mtu hataishi kwa mkate pekee, bali kwa kila Neno." Si sehemu ya Neno; bali kila Neno, Hilo lote. "Kila Neno litokalo katika kinywa cha Mungu," hilo ndilo mtu huishi kwalo. Yeye ni yakini yako katika maisha yako, Yeye pia ni Nyota yako ya Kaskazini.

⁷² Mnajua, inatubidi kuwa na kitu, kingine, kutatua mwisho wa ugomvi.

⁷³ Mnajua, kulikuwa na wakati ambapo mwenendo wa tabia za mezani ziliegemea juu ya kile mwanamke alisema. Ninaamini

jina lake lilikuwa Emily Post. Huenda nikakosea kwa hilo. Nafikiri hiyo ni kweli, Emily Post. Sijali kama Emily Post alisema, “Chukua kisu chako na ule ma—maharagwe nacho,” hizo zilikuwa ni taratibu. Kwa nini? Alikuwa ndiye yakini ya adabu mezani. Hiyo ni kweli. Kama alisema, “Kula hayo kwa mikono yako,” unayala kwa mikono yako. Kwa nini? Taifa hili lilimfanya kuwa yakini, kwa adabu za mezani. Naam, bwana.

⁷⁴ Kulikuwa na wakati ambapo Ujerumani ulikuwa na ya—yakini, na hiyo ilikuwa ni Hitler. Ilikuwa ni yakini. Sijali kile mtu yeyote mwingine alichosema, wakati Hitler alisema, “Fanya hiyo,” unafanya hiyo. Afadhali ufanye. Yeye ndiye neno la mwisho. Hitler alikuwa.

⁷⁵ Kulikuwa na wakati ambapo Rumi ilikuwa na yakini, na hiyo ilikuwa ni Mussolini, mtawala wa kimabavu. Mtu aliendesha motokaa dakika moja mapema kwake, alimpiga risasi katika motokaa yake na kumvuta nje, kasema, “Sikusema dakika moja mapema, nilisema uwe hapa kwenye wakati.” Yakini! Chochote alichosema, iliwabidi kukifanya. Ilibidi igeuke. Alisema yeye angeufanya ulimwengu wote ugeuke kwa neno lake. Unageuka kwa Neno la Mungu!

⁷⁶ Kulikuwa na wakati ambapo Misri ilikuwa na yakini. Ilikuwa ni Farao. Nilienda huko Misri wakati mmoja, ili tu kuona sehemu hizo. Na inakubidi kuchimba chini futi ishirini kuvipata viti vya enzi ambavyo walikalia, mfalme wa Rumi; wakati nilipokuwa Rumi na huko chini Misri.

⁷⁷ Unaona, yote iligeuka kuwa vumbi la kihistoria, kwa sababu ilikuwa ni aina ya yakini isiyofaa. Hiyo ni kweli. Haifai. Ilishindwa. Zilikuwa ni yakini zilizotengenezwa na mwanadamu. Na kila yakini iliyotengenezwa na mwanadamu na kila mafanikio yaliyofanywa na mwanadamu hayana budi kuingia mavumbini. Hayana budi kuingia mavumbini. Ni aina isiyofaa, kwa hiyo inashindwa.

⁷⁸ Hebu wazia tu taifa letu. Wakati tukiingia katika shida, mtu akitenda jambo fulani, na wanalisisikiliza hapa katika ma—mahakama ndogo ya mji, mahakama fulani ya polisi, kisha linaendelea, linaendelea, na hatimaye linakuja kwenye Mahakama Kuu. Sasa, Mahakama Kuu ndiyo yakini ya taifa. Hiyo hilitatua. Sasa, huko Kanada, rafiki zetu kutoka Kanada wanaweza kwenda, kutoka Kanada, kwenda kwa Malkia. Lakini katika Marekani, ni Mahakama Kuu. Hiyo ndiyo yakini. Wakati mwingine hatuyapendi maamuzi yao, lakini inatubidi kuyasikiliza hata hivyo. Naam, bwana. Hatukubaliani nayo, hatupendi uamuzi wakati mwingine, bali ndiyo yakini ya taifa hili. Taifa limefungwa kwayo. Ndiyo mwisho wa mabishano yote. Wakati hiyo Mahakama Kuu ikisema, “Una hatia,” una hatia. Lazima tuwe nayo; kama hatunayo, hatuna taifa. Vipi

iwapo hatukuwa na kitu kama hicho? Hakika. Kuna yakini kwa kila kitu.

⁷⁹ Kuna yakini katika mchezo wa mpira. Huyu ni mwamuzi. Kweli. Na kama akisema, “Ni dafrao,” hivyo ndivyo lilivyo. Haijalishi kile unachosema, kile ninachofikiria, jinsi nilivyoliona, jinsi ulivyoliona. Ni kile alichosema. Ni yakini. Kama akisema, “Dafrao,” lazima ukubaliane nalo, maana hivyo ndivyo litakavyoandikwa, “dafrao.” Vipi kama hakukuwa na mwamuzi, sasa ni nani angekuwa sahihi? Mmoja alisema, “lilikuwa ni dafrao,” yule mwingine akasema, “haikuwa dafrao; ulikuwa ni mpira, ulikuwa ni...” Mbona, mngekuwa na machafukio. Msingejua la kufanya.

⁸⁰ Hapana budi pawe na mahali ambapo neno la mtu fulani ni yakini. Amina. Ninajisikia vizuri sana sasa. Utukufu! Haleluya! Lazima kuwe na kitu ambacho ni mwisho. Nina furaha sana kwa hilo. Loo, sasa, kuna mtu anayeweza kusema, “Ni dhambi,” ama, “Si dhambi.” Nina furaha sana kwa hilo. Nina furaha sana kwa ajili ya yakini. Hakuna kubishana, hakuna haja ya kubishana. Mwamuzi alisema, “dafrao,” ndivyo ilivyo; weka hilo niani mwako, “ni dafrao,” na uendele. Mungu anaposema kitu chochote, hivyo ndivyo kilivyo! Hakuna haja ya kubishana juu yake. Hicho ndicho kilicho. Yeye alisema hivyo. Hicho ndicho yakini ya Mkristo, hiyo ni ikiwa yeye ni Mkristo. Mungu alisema, “Ifanye kwa njia *hii*,” hiyo ndiyo njia inayopaswa kufanywa. Hakuna kubishana, “Vema,” sema, “haikuwa.” Hakuna kitu juu yake. Mungu alisema hivyo, hilo latosha! Hiyo ndiyo yakini kwa mwaminio halisi. Naam.

⁸¹ Vipi kama hakukuwa na kitu kama hicho, tungekuwa wapi? Je! Methodisti ingekuwa sahihi, Baptisti, Presbiteri, Lutheri, ama ni nini ingekuwa sahihi? Unaona, tungekuwa na, hiyo ndiyo sababu m—mngekuwa na vurugu. Na hiyo ndiyo sababu. Wamelegea kwenye hiyo yakini, hiyo ndiyo sababu wanapotoka na hizi nyota zingine.

⁸² Lakini kuna yakini. Hakuna budi kuweko yakini. Lazima kuwe na yakini. Na kuna yakini. Hiyo ni Neno. Na kile wengine wasemacho, hakijalishi. Naam, bwana.

⁸³ Sasa, ikiwa hatukuwa na mwamuzi katika mchezo wa mpira, kila mtu angekuwa akivuta nywele za mwenzake, na kuzozana na kupigana. Mnaona? Hiyo ndiyo sababu tunahitaji yakini katika Ukristo, acheni huku kuvuta nywele, na kuzozana na kupigana. Unaona? Neno lililisema, na hilo latosha. Usiongeze Kwake wala kuondoa Kwake. Liache tu jinsi lilivyo.

⁸⁴ Unajua, kuna yakini kwa magari barabarani, hiyo ni taa ya kusimamisha, alama ya barabarani. Vipi kama asubuhi moja haifanyi kazi? Loo, jamani! Hivi uliwahi kuingia katika moja ya hizo? Mimi nimewahi. Hapana shaka, dereva yeyote amewahi. Vipi kama taa hiyo ya kusimamisha haifanyi kazi?

Basi kila mtu anazozana. Wanaendesha motokaa huko juu, na mmoja anasema, “Nilitangulia hapa,” huyo mwingine anasema, “Hebu nikwambie jambo fulani, inanibidi kuenda kazini!” Loo, jamani! Hao wanawake wakipunga vitabu vidogo vya mifukoni, nao wanaume wakipigana kwa makonde, nawe uzungumze kuhusu vurugu! Hapana budi pawe na yakini, kitu fulani kinasema, “*Hii* ni sahihi,” na hiyo yatosha. Wakati nuru hiyo iliposema, “simama,” inamaanisha simama. Ikisema, “nenda,” inamaanisha nenda. Kama sivyo, uko katika matatizo.

⁸⁵ Na hivyo ndivyo ilivyo katika maisha ya Kikristo. Pana mahali pa kusimama, na pana mahali pa kwenda. Neno la Mungu ndilo hiyo yakini. Hilo ni Kristo. Naam, bwana. Ikiwa wewe. . .

⁸⁶ Kama alama za trafiki haziwaki, basi tuna msongamano wa magari. Nami ninafikiri huo ndio tunao kule juu kwenye makao makuu ya kidini leo; msongamano wa magari, wa wanaojifanya waaminio, wasioamini, na kila kitu kimesongamana pamoja. Una msongamano wa magari tu. Kwa nini? Hawana yakini yoyote. Mmoja anasema, “Vema, sisi ni. . . Sisi ndio yakini.” Huyo mwingine anasema, “Sisi ndio yakini.”

⁸⁷ Mungu ndiye Yakini. Yeye alisema, “Hebu kila yakini, mbali na Yangu, iwe uongo. Yangu ndiyo Kweli!” Kwa hiyo, hiyo hapo yakini kwa Ukristo. Huo ndio mwisho wa mabishano yote. Biblia ilisema hivyo, hiyo inafanya Hilo kuwa sahihi. Naam, bwana. Lazima kuwe na yakini katika kila jambo.

⁸⁸ Mengine tu kama makanisa leo hii, mengi ya makanisa yanayo yakini yao yenyewe. Kila moja lina yake, kitu kama siku za waamuzi, kila mtu alifanya vile alivyofikiria ilikuwa sahihi. Bali hiyo si sahihi. Unaona, hapo ni wakati Neno la Mungu na manabii hawakuwepo. Neno ndilo yakini. Walikuwa na yakini yao yenyewe. Kila mmoja anasema wao ndio Kweli na njia, “Sisi ndio Kweli na njia.”

⁸⁹ Bali Yesu alisema Yeye alikuwa ndiye Kweli na Njia, “Kweli, Njia, na Nuru.” Je! hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Vema, basi, Yeye ni Neno, basi hiyo hapo yakini. Na yakini za kimadhehebu, hakuna kitu kwake; ni makosa, achana nayo.

⁹⁰ Sasa, mtu hufanya mema machoni pake mwenyewe, lakini Mungu anayo njia kwake kufanya hayo. Unaona, wakati Mungu na Neno Lake na manabii Wake hawakuwepo, kila mtu alifanya tu alivyotaka kufanya.

⁹¹ Na hiyo ndiyo imekuwepo katika siku hii, kila mmoja anasema, “Mimi—mimi ni mfuasi wa *hili*.” Je! wewe ni Mkristo? “Mimi ni Mpresbiteri.” Je! wewe ni Mkristo? Ninakuuliza. Msichana mmoja alisema, “Nakupa kufahamu, ninawasha mshumaa kila usiku.” Mtu mwingine alisema, katika mstari wa maombi, nilimwuliza kama alikuwa ni Mkristo, kasema, “Mimi

ni Mwamerika. Unathubutuje!” Kana kwamba hiyo ina chochote kuhusiana na Hilo? Unaona, wamefungwa kwenye taifa. Yule mwingine amefungwa kwenye dhehebu, mifumo ya imani.

⁹² Lakini *Mkristo* linamaanisha “Kama Kristo.” Na njia pekee uwezayo kuwa kama Kristo ni kwake Kristo Neno kuwa ndani yako. Huo ndio mkataa. Naam. Niliona hili kabla sijaongoka, na nina furaha Mungu alinishika kabla ya kanisa kunishika. Kwa hiyo nilijua wakati mimi . . .

⁹³ Mhudumu mzuri wa Kibaptisti, Ndugu Naylor, yuko Utukufuni leo, alishuka chini, akazungumza nami. Na, loo, wapo watu wengi waliozungumza nami wakati ni—nilipokuwa nikijaribu kumtafuta Mungu. Mhubiri wa Sabato alinitaka nijiunge nao, na kadhalika. Lakini niliona kwamba kama nilikuwa ninaenda kuwa Mkristo, ni—nisingeweza kusema, “Sasa mimi ni wa Sabato.” Sasa, hiyo ni sawa. “Mimi ni Mbaptisti.” Ni sawa, unaona, ila ilinibidi kuwa na kitu chenye hakikisho zaidi kidogo kuliko hicho. Ni—nisingeweza kutumainia, kwa sababu kila mmoja alikuwa anayumbayumba.

⁹⁴ Nikawaza, “Yupo mtu mahali fulani, huna budi kuwa na kitu kilicho kweli, mahali fulani.”

⁹⁵ Kwa hiyo nilihitaji yakini, kwa hiyo nikachukua moja, Neno la Mungu. Kwa hiyo nilisoma katika Neno kwamba Yeye ni Neno, Yohana Mtakatifu 1. “Na juu ya yakini hii, nitalijenga Kanisa Langu.” Hiyo ni kweli, kwa hiyo nilimchukua Yeye kwenye Neno Lake. Ufunuo 22:19 ilisema, “Yeyote atakayeondoa Neno moja kutoka kwenye Hii, ama kuongezea neno moja Kwake.” Hiyo ndiyo yakini. Huo ndio mwisho wa ugomvi wote. *Hii* ndiyo yakini. “Yeyote aondaye chochote kutoka kwa Hiyo, au kuongeza chochote kwa Hiyo,” Mungu alisema, “Nitaondoa tu sehemu yake kutoka kwenye Kitabu cha Uzima,” kwa hiyo Hiyo ilibidi iwe ndiyo yakini. Pia Yesu alisema kwamba, “Mtu hataishi kwa mkate pekee, bali kwa kila Neno.” Ndipo nikajua hii “kila Neno” ilibidi iwe hivyo. Kasema, “Amri juu ya amri, na mstari juu ya mstari.” Hivyo ndivyo Hilo halina budi kuja, jinsi tu lilivyoandikwa.

⁹⁶ Ndipo akasema, “Mkikaa ndani Yangu,” Yeye ni Neno, “Maneno Yangu yakae ndani yenu, mnaweza kuomba mtakalo.” Nilijua basi ikiwa Ukristo ulikuwa ni Neno la Mungu. Na Yeye alikuwa ni Neno; na kwa kulikubali Neno, Neno liliishi kupitia Yeye, basi ninajua, “Mkikaa ndani Yangu, na Neno Langu ndani yenu, ombeni mtakalo.” Na ikiwa uko ndani ya Neno na sehemu ya Neno, utaomba tu kile Neno linalokuambia uombe. Ijue siku unayoishi, basi, ndipo uombe ipasavyo.

⁹⁷ Kwa hiyo basi, turudi kwenye somo, inafanya... Nikizungumza hili sasa binafsi, bali nimefungwa. Nimefungwa kwa Yesu Kristo, Kwake, kwa Neno Lake. Yeye ndiye yakini yangu.

⁹⁸ Niligundua kwamba madhehebu haya yote na kadhalika yalikuwa na yakini yao. Kila moja, kila moja, wana yakini yao wenyewe.

⁹⁹ Katoliki, huyo papa akisema jambo, hilo ndilo. Hiyo ndiyo yakini ya kanisa Katoliki. Sijali kile kasisi asemacho, kile askofu asemacho, kile kadinali asemacho; papa anapolisema, hilo ndilo. Hiyo ndiyo yakini. Ni kweli.

¹⁰⁰ Katika kanisa la Methodisti na mengi ya madhehebu ya Kiprotestanti, kile askofu asemacho, hicho ndicho yakini. Hicho chatosha. Kile kanuni ya imani isemacho, hicho ndicho yakini.

¹⁰¹ Katika Pentekoste, ni kile mwangalizi mkuu asemacho, kama mnaweza kuwa na mtu huyu kwa ajili ya uamsho, au la. Hicho ndicho yakini. Usipokubaliana na maneno yake, unatupwa nje ya dhehebu hilo. Unaona, Neno halizingatiwi hata kidogo. Unaona? Unapata yakini hizi, kila mmoja akiwa na yakini yake mwenyewe.

¹⁰² Lakini, unajua, sisemi hili kwa njia ya makufuru. Ninalisema kwa ajili ya kweli. Ninajisikia namna ile aliyojisikia Paulo, wakati aliposema, katika Matendo 20:24, “Hakuna moja ya mambo haya linalonishtua.” “Nimekusudia nisijue neno lolote kwenu; ila Yesu Kristo, Naye amesulubiwa.” Sisumbuliwi kuhusu hizi yakini, kama ni papa, askofu, ama mwangalizi mkuu, ama mshauri, au mfumo, ama chochote kile, hakuna moja ya mambo haya linalonishtua. Sijali kama wakisema, “Vema, sisi—sisi hatuta-...” Hiyo haileti tofauti yoyote. Nimeazimia nisijue chochote ila Yesu Kristo, Neno Lake lililodhihirishwa miongoni mwetu. Nimefungwa kwenye Hilo. Hiyo ndiyo nanga yangu. Nimetia nanga kwenye Hilo.

¹⁰³ “Tangu mimi...” Paulo alisema, “Tangu nilipokutana na Yeye, barabarani, nimegeuka. Nime... Yeye alininyoosha.”

¹⁰⁴ Jamani, jinsi Yeye alivyoniweka sawa! Ni kunyoosha jinsi gani kulikombidi Yeye kunifanyia. Lakini tangu Yeye aliponinyoosha, nilifungwa kwa Hilo. Niliona Neno lilikuwa Kweli, kila kitu kinyume Nalo lilikuwa kosa.

¹⁰⁵ Unajua nini? Alikuwa na kusudi katika kuniokoa mimi. Alikuwa na kusudi katika kukuokoa wewe. Nami nimeazimu, kwa mapenzi Yake, kufanya mapenzi Yake. Sababu ya Yeye kufanya hilo, sijui ni kwa nini Yeye alifanya hilo.

¹⁰⁶ “Usiongeze kwenye Hilo wala kuondoa kwenye Hilo!” Kama nilivyosema, Ufunuo 22:19 ilisema usifanye hivyo. Kama Yeye ndiye yakini yetu, haiwezi kuwa vinginevyo. Hakuna njia yoyote kwake kuwa vinginevyo. Yeye hana budi kuwa ndiye yakini, Neno la Mwisho.

¹⁰⁷ Unajua, kulikuwa na mamilioni katika dhambi wakati nilipookoka. Alikuwa na kusudi katika kuniokoa. Mimi ni wa kipekee miongoni mwa ndugu, mara nyingi; ninaamini katika

kuchaguliwa kimbele, uzao wa nyoka, ubatizo katika Jina la Yesu Kristo, na mambo haya yote mengine ambayo yanaonekana kuwa... na maono, na nguvu za Kristo zikirudi, na kukemea madhehebu na kadhalika. Mimi ndiye wa kipekee, lakini Yeye alikuwa na sababu kuniokoa, kusudi la kufanya hivyo. Aliniokoa wakati kulikuwa na mamilioni ya wengine katika dhambi, lakini Yeye aliniokoa kwa kusudi fulani. Kulikuwa na watu wenye elimu, kulikuwa na watu werevu, kulikuwa na wanatheolojia, kulikuwapo na maaskofu na madaktari, na kadhalika, uwanjani, wakati Yeye aliponiokoa, bali Yeye aliniokoa kwa sababu fulani.

¹⁰⁸ Basi ninaona Neno ndilo yakini, nami nimefungwa Kwalo, na nimeazimu sitajua chochote kingine ila Yesu Kristo, na Yeye amesulubiwa. Alikuwa na sababu kwa hilo, na mimi nimeazimu kushikilia sababu hiyo. Haijalishi kile mtu yeyote mwingine asemacho, sivunji ushirika nao wala kuwadhalilisha, lakini ninajua kile nilichofungiwa. Alinitaka hivi. Aliniumba hivi. Niliumbwa hivyo kwa kusudi. Ilinibidi kuumbwa na sifa hizi zote, na kadhalika, na huku kutokuwa na thamani kote, ili Yeye aweze kuichimbua kutoka kwangu, aweke Kitu fulani mle ndani; icho kilikuwa ni Neno Lake. Nami nimeazimu sitajua chochote kingine ila Kristo.

¹⁰⁹ Kifo cha Kristo kilikuwa yakini. Kilikuwa yakini. Kilikuwa ndicho mwisho wa hofu zote kwao walioogopa kifo. Kifo Chake ni yakini, basi.

¹¹⁰ Watu wanaogopa kifo. Hata Ayubu aliogopa kifo. Lakini alipoliona ono! Alijua kila kitu kilitoweka; familia yake, wa—watoto wake. Hata mke wake alikuwa amemgeuka, kwa sababu m—mnuko wake wa ninii yake—wa majipu yake; aliketi nje ya nyumba yake, kwenye lundo la majivu, akiyaparua ma—majipu yake. Naye mke wake hata alisema, “Kwa nini usimlaani Mungu, na ufe kifo?”

Akasema, “Wewe wanena kama mwanamke mpumbavu.” Unaona?

¹¹¹ Halafu wakati Elihu alipozungumza naye... Baadhi ya siku hizi, ninataka kuwachambulia jina hilo, Elihu, na kuwaonyesha ilikuwa ni Kristo.

¹¹² Wakati alipokuwa na hali hii, na kila kitu kilikuwa kimemwendea kinyume, ndipo alipoona ono la Yule Mwenye haki. Alitamani kumpata Mtu aliyeweza kusimama katika pengo kwa ajili yake; aweke mikono Yake juu ya mtu mwenye dhambi na Mungu Mtakatifu, na kusimama njiani. Ndipo Mungu akamwacha aone Hilo, umbali wa miaka elfu nne. Lilikuwa yakini yake. Alisimama na kujitikisa. Haleluya!

¹¹³ Wakati mtu anapoogopa kufa, simama na ujitikise mwenyewe, angalia kwenye Neno na uone kile ono la Mungu lilicho.

¹¹⁴ Aliliona hilo ono, akasema, “Ninajua Mkombozi wangu yu hai, na katika siku za mwisho Yeye atasimama juu ya nchi. Nami ninajifunganisha kwa hilo! Ingawa mabuu ya ngozi yanauharibu mwili huu, hata hivyo katika mwili wangu nitamwona Mungu; Ambaye nitamwona mwenyewe. Nimefungwa kwa hilo,” akasema. Aliliona. Lilikuwa ni ahadi ya Mungu.

¹¹⁵ Aliangalia kupitia kanuni za maumbile. Kama nilivyokuwa nikiwaambieni kuhusu mwendeleo wa kanuni ya maumbile, mwendeleo wa Neno, mwendeleo wa kazi ya Mungu, kila kitu ni mwendeleo. Alikuwa ameuliza, katika Ayubu 14. Alisema, “Kuna matumaini katika mti, ukifa; ua, likifa; na kadhalika. Lakini,” kasema, “mwanadamu hulala chini, naye hutoa roho, huharibika tu. Wanawe huja kumtolea heshima, wala yeye hajui. Loo,” ndipo akasema, “laiti Wewe ungenificha kaburini, unifiche mbali na kunilinda mahali pa siri, hata ghadhabu Zako zitakapopita!” Aliogopa kifo.

¹¹⁶ Lakini wakati alipoona kimbele, akiwa ni nabii, aliona kufufuka kwa Yesu Kristo, alipaza sauti, “Mkombozi wangu yu hai!” Tazama, alimwita, “Mkombozi.” Tazama. “Ninajua Mkombozi wangu yu hai, na katika siku za mwisho Yeye atasimama juu ya nchi; ingawa baada ya mabuu ya ngozi yangu kuharibu mwili huu, hata hivyo katika mwili wangu nitamwona Mungu.” Mungu na Mkombozi walikuwa ni kitu kile kile, Mungu na mwanadamu wakifanyika kitu kimoja. “Nitamwona Mungu; Ambaye nitamwona mwenyewe, macho yangu yatatazama, na si mwingine.” Amina.

¹¹⁷ Si mtu yeyote mwingine bali huyo Mkombozi, Mungu, huyo Ndiye macho yangu yanamwona. Yeye ni yakini. Yeye ndiye yakini. Yeye huondolea mbali hofu zote kutoka kwa kifo. Yeye huchukua hofu zote.

¹¹⁸ Katika Waebrania, mlango wa pili, kifungu cha 14 na cha 15, tazama. Alichukua umbo la mwanadamu, kufa kama mwanadamu, kwa ajili ya wote. Alichukua umbo la mwanadamu. Mkombozi huyu alishuka chini na akafanyika mwanadamu, ili Yeye aweze kufa, Mtu mmoja, kwa ajili ya watu wote. Loo, alifanyaje jambo hilo? Ni kwa nini Mungu akafanyika mwanadamu? Kulipa adhabu ya mwanadamu.

¹¹⁹ Lakini, kwenye asubuhi ya Pasaka, Yeye alikuja na funguo za kifo, kuzimu, na kaburi. Amina. Mungu, Yule aliyeweza kufa msalabani, nayo makaburi hayakuweza kumshikilia; hakuna kitu, kuzimu kusingeweza kumshikilia Huyo. Hakuna kilichoweza kumshikilia. Alifufuka. Alikuwa na funguo. Alifufuka, Mshindi, kwa sababu Yeye alishinda yote kifo, kuzimu, kaburi. Wakati Yeye alipokuwa duniani, alishinda ugonjwa. Alishinda kila kitu. Alishinda ushirikina. Alishinda kila kitu kilichokuwepo cha kushindwa. Na akatoka na kifo,

kuzimu, na kaburi, funguo zikilia ubavuni Mwake; na akapaa Juu, na kuwapa wanadamu vipawa, na kurudi kwenye Siku ya Pentekoste na kuzikabidhi Petro, Kanisa. Amina. Yeye ndiye yakini yetu. Hofu zote za kifo . . . Kwa sababu Yeye anaishi, nasi twaishi pia.

¹²⁰ Warumi 8:1, “Basi tukiisha kuhesabiwa haki kwa imani, tunayo amani kwa Mungu kwa njia ya Bwana wetu Yesu Kristo.” Tunaona, ninaamini hiyo ni Warumi 5, tunaona. Pia—pia Yeye ndiye haki yetu. Mungu alimfufua katika siku ya tatu, kuhesabia haki imani yetu, kwamba tunaamini. Basi Yeye alimfufua, kuhesabia haki imani yetu. Alifanya nini basi? Alimtuma Yeye arudi, Mwenye kuhesabia haki, kwa sababu imani yetu inaamini hilo. Roho Mtakatifu, Kristo, akaingia ndani yake, kwa ajili ya kutuhesabia haki, kwa sababu tumefufuka kutoka mautini kuingia Uzimani. Na sasa sisi ni wana na binti za Mungu, tumeketi katika mahali pa Mbinguni katika Kristo Yesu, ametuhesabia haki kwa kufufuka Kwake.

¹²¹ Hilo linatupa kuhesabiwa haki, kujua, pamoja na—pamoja na arabuni ya wokovu wetu ndani yetu sasa, Uhai wenyewe wa Kristo ukidunda ndani yetu. Na tungewezaje basi kulikana Neno? Ambalo, Yeye ndiye Neno ambalo hutupatia . . . uhakika huu. Roho Mtakatifu yupo pale. Ni nini Huyu? Angali ni ile Nyota ya Kaskazini, Kristo ndiye ile Nyota ya Kaskazini. Naye Roho Mtakatifu ndiye kule kuhesabiwa haki kunakomwelekeza mwaminio moja kwa moja kwenye Nyota ya Kaskazini. Kweli.

¹²² Roho Mtakatifu sikuzote ataelekeza kwenye Neno. Kama akielekeza kwenye kanuni ya imani au dhehebu, si Roho Mtakatifu. Asingeweza kufanya hilo, kuelekeza mbali na Neno Lake, wakati Yeye alikufa ili kulithibitisha Neno hilo na kulifanya Neno hilo hakika. Amina. Alikufa ili aweze kuja, Mwenyewe, ndani ya Neno hilo. Yeye ndiye Uhai unaohuisha ambao hulifanya Neno hilo kuishi tena. Hilo lilikuwa ndilo kusudi Lake la kufa, ili aweze bado kujionyesha Mwenyewe kupitia Kanisa Lake, na kufanya kila Neno, kupitia kila wakati, kutenda vile hasa Hilo linavyopaswa kutenda.

¹²³ Yeye ndiye nguvu tendaji za mitambo. Mitambo ya Kanisa, ni kitu gani? Mitume, manabii, walimu, kadhalika. Na Yeye ndiye nguvu tendaji zinazoendesha huo. Nao huendeshwa na nguvu fulani ambazo zinaitwa kama . . . Yeye, Yeye ndiye Moto ambao huiwasha gesi. Yeye ndiye Moto ulio ndani ya chemba ya mwako, ambaye wakati ge—gesi, lile Ne—Neno linapomiminwa juu ya chemba ya mwako, Yeye ndiye Yule ambaye hutia moto. Yeye ndiye Yule ambaye huithibitisha. Yeye ndiye nguvu za kufufuka. Yeye ni Mungu. Yeye, Yeye ndiye Moto, huo ndio alio Yeye.

¹²⁴ “Bila mabishano,” ilisema Timotheo wa Kwanza 3:16, “siri ya utauwa ni kuu; kwa kuwa Mungu alidhihirishwa katika mwili, akaonekana na malaika, akapokelewa juu utukufuni.”

Yeye alikuwa ni Mungu, aliyekuja kuchukua mahali pa wenye dhambi. Naam, bwana. Na wakati Yeye, Mungu, alipomfufua Yeye kwenye—kwenye siku ya tatu, ilikuwa ni kwa ajili ya kutuhesabia haki. Hivyo basi, akainuliwa katika mkono wa kuume wa Ukuu huko Juu, Yeye ni Mwombezi, kufanya maombezi juu ya ninii yetu...kwa ajili ya udhaifu wetu, tunapoukiri Kwake, na kufa kwa nafsi zetu; akiweka Neno Lake tena ndani yetu, ahadi. Nayo imani yetu hulifanya Neno hilo kuishi, kwa sababu Kristo yuko ndani yetu, mhuishaji wa Neno.

¹²⁵ Laiti kanisa lingaliweza kuona hilo, mabishano yote na ugomvi ungeisha! Hiyo ingekuwa ndiyo Mahakama Kuu. Hiyo ndiyo Nyota ya Kaskazini. Haleluya! Huo ndio mwisho wa ugomvi wote. Huo ndio mwisho wa maswali yote. Huo ndio mwisho wa kila kitu. “Mungu alisema hivyo,” hiyo ndiyo Yakini. Jifungamanishe mwenyewe Kwayo. Paulo alisema, “Hakuna kitu kilichopo, wala kitakachokuwepo, kifo, ugonjwa, uchi, hatari, hakuna kitu kiwezacho kututenga na Hiyo.” Tumejifunga kwenye yakini. Kasema, “Kwangu mimi kuishi ni—ni Kristo, na kufa ni faida.” Hakuna kitu kingine kinachoshikilia ila Hiyo hapo. Hiyo ndiyo yakini.

¹²⁶ Yeye ndiye Yakini yetu kwa sababu tunalo hakikisho la ufufuo, kwa sababu Yeye amefufuka ndani yetu. Tunajuaje? Yeye anaishi. Yeye anafanya hapa hasa yale aliyofanya wakati Yeye alipokuwa hapa duniani. Yeye ni Nguzo ile ile ya Moto, tunayo picha yake pale. Ni yeye yule yule Kanisani. Yupo hapa leo hii, na katika mwili huu Yeye anatenda na kufanya hasa jinsi alivyofanya wakati ule.

¹²⁷ Kama uhai wa tikitimaji ukiwekwa ndani ya boga, hautazaa boga jingine; hauwezi, maana utakuwa ni tikitimaji, kwani uhai ulio ndani yake ni tikitimaji. “Na ikiwa ninii Yangu... Mkikaa ndani Yangu na maneno Yangu ndani yenu, ombeni mtakalo!” Utakuwa na tikitimaji. Amina. Yakini, ninajua ni Kweli. Nimeifunga nafsi yangu katika hiyo, nami ninajua ni Kweli. Neno la Mungu, Yeye ni Yakini yetu.

¹²⁸ Wathesalonike wa Pili, mlango wa pili, tunasoma hilo. “Tutanyakuliwa juu pamoja na wapendwa wetu, kumlaki hewani.” Loo, jinsi moyo wangu unavyodunda kwa kila Neno katika Kitabu Chake, “Amina.” Mungu alisema, “Tutanyakuliwa juu hewani, kukutana na wapendwa wetu.” “Amina,” kasema Neno chini moyoni mwangu, kwa kuwa Neno liko mle ndani.

¹²⁹ “Nimelificha Neno Lako moyoni mwangu, Bwana, ili nisikutende dhambi. Nimeyafunga juu ya vidole vyangu, juu ya mhimili wa kitanda changu. Wewe daima uko mbele zangu. Sitatikisika.”

¹³⁰ “Naam, nijapotembea kupitia bonde la kivuli cha mauti, sitaogopa uovu wowote, kwa kuwa Wewe ni Yakini yangu.

Nitateremka kupitia hapo, na Wewe utanivuta unitoe. Ninaingia katika maji yenye kilindi kwa meli yangu, Wewe uta... Wewe ndiye nanga yangu. Amina. Uko nyuma ya pazia kule. Wewe ndiye Yule Ambaye ataniongoza kupitia kwenye dhoruba. Wewe ndiye Yule atakayekuwa Huko, nanga yangu Utukufuni, ninapofikia chini kwenye vivuli vya bonde, vivuli vya mauti." Nikifika chini Yordani, inaponibidi kuvuka, Yeye ndiye Yakini yangu. Nimefungwa kwake Yule aliyefufuka upande ule mwingine, Yeye atanivuta kupitia maji yenye hatari. "Sitaogopa uovu wowote, kwa kuwa Wewe uko pamoja nami." Amina. Acha dhoruba zivume, uhai, mauti, chochote kilichopo; hakuna kitu kitakachotenga. Nimefungwa kwenye Nguzo hiyo.

¹³¹ Nguzo hiyo inashikilia. Inashikilia ndani ya pazia. Iilitiwa nanga. Ilifungwa kwa Mungu huko ng'ambo. Ilifungwa kwa moyo wangu. Roho Mtakatifu ndiye hunichochea kwenye ahadi hiyo. "MIMI NIKO!" Sio "Nitakuwepo," "Nilikuwepo," "Siku moja nitakuwepo." "Mimi ndimi Ufufuo na Uzima," asema Mungu. "Yeye aniaminiye Mimi, ajapokufa, hata hivyo ataishi. Na yeyote aishiye na kuniadini Mimi, hatakufa kamwe."

¹³² Acha kifo kitende chochote kitakacho, kamwe hakitanisumbua, kwa sababu, nimeshawishika, nimeshawishika kwamba hata katika ugonjwa unaoweza kunichukua, ama risasi kutoka kwenye bunduki, huenda ikanichukua, siku moja, sijui itakuwa kitu gani, inaleta tofauti gani kwangu? "Kwangu mimi kuishi ni Kristo, na kufa ni faida." Loo, jamani! Kwa sababu, nimeazimu nimjue Yeye ameketi huko ng'ambo ya mto wa mauti, ambapo Yeye atanivuta kuniingiza katika Uwepo Wake siku moja. Nimehesabiwa haki kwa haki Yake, niliyokubali kuhusu kifo Chake msalabani, Mungu akifanyika mwili miongoni mwetu; angali ni mwili ndani yetu, angali ni Roho katika miili yetu. Amina.

¹³³ Yeye ndiye Yakini yangu. Yeye ndiye yote kwangu. Chochote nje ya hiyo, sina chochote mkononi ninacholeta. Sijui chochote kando na Kristo, na Yeye amesulubiwa; sitaki kusikia chochote kingine ila Kristo, na Yeye amesulubiwa. Moyo wangu unasema "amina" kwa kila moja ya ahadi Yake. Hiyo ndiyo sababu ninajua Roho Wake Mtakatifu ni dira, Hiyo huniongoza kwenye Neno.

¹³⁴ Kamwe hakuna moja ya hayo maono lililowahi kuniambia chochote ila kilicho sahihi katika Neno. Loo, hapo ndipo nilipopata hakikisho langu, ndugu. Usiku ule aliponiambia kuhusu hilo, nimeyaangalia hayo maono. Nami nitaita usikivu wenu, hivi ono hilo limewahi kusema chochote ambacho kilikuwa kinyume na Neno? Hakuna wakati hilo limewahi kukosea. Kwa nini? Ni Mungu. Hiyo ndiyo nguzo yangu ya kufungiwa.

¹³⁵ Tena ninajua, asubuhi moja, katika ono, niliwaona wapendwa wangu huko ng'ambo ya mto. Ipo. Sina budi kwenda katika Nchi hiyo ya ahadi. Sina budi kukutana huko siku moja. Naam, kweli.

¹³⁶ Yeye ni Yakini yangu. Yeye ni Jua langu. Yeye ni Uzima wangu. Yeye ni nguzo yangu ya kufungiwa, Nyota yangu ya Kaskazini. Yeye ndiye yote ninayoweza kuwazia kuwa, Yeye ni hayo kwangu. Yeye ni Uzima wangu.

¹³⁷ Madhehebu, kwangu. . . Si kuudhi hisia zenu; sitaki kufanya hayo. Lakini Neno ni kama upanga ukatao kuwili, hauwezi kusukuma bila kukata, unaona, hasa wakati unakata kwenye giza. Tazama, madhehebu ni kama nyota zingine, zinageuka na mzunguko wa ulimwengu. Hiyo ni kweli. Kila njia ulimwengu uendayo, wanawaacha wanawake wao kukata nywele zao, kuvaa kaptura, na kila kitu kingine, inasonga tu na Hollywood na kila kitu kingine. Bali, loo, ndugu, *Hilo* lingali linabaki ndilo Kweli, hilo Neno lisilotikisika la Mungu lingali Kweli! Ni Yakini yangu. Kile Hilo lisemacho ni Kweli. Acha dhehebu lihamie popote watakapo. Wanataka kufedhehesha Jina la Yesu Kristo, kwa cheo, hiyo ni juu yao. Ila, kwangu mimi, "Hapana Jina jingine chini ya Mbingu walilopewa wanadamu, liwapasalo kuokolewa kwalo." Kwangu mimi, hilo ndilo Neno la msingi, hapo ndipo palipo na jiwe la pembeni. Sitaki kuhama na dhehebu lolote.

¹³⁸ Ninayo Dira yangu hapa ndani yangu, Roho Mtakatifu, hunielekeza moja kwa moja kwenye Yakini. "Kwa kuwa mbingu na dunia zote zitapita, bali Maneno Yangu hayatapita kamwe." Nami nimeficha Hilo moyoni mwangu, naye Roho Mtakatifu alinielekeza moja kwa moja kwa Hilo. Nimeazimia nisijue chochote kingine. Hilo ndilo Yakini yangu. Liache tu liwe hivyo. Hivyo ndivyo ninavyolitaka. Loo, jamani! Sasa, ndugu, dada, ifanye Yakini yako ndani Yake. Naam, bwana.

¹³⁹ Katika wakati wa shida niliyokuwa nayo hapa si muda mrefu uliopita, nilimpoteza mke wangu, watoto, kila kitu. Mtu fulani aliniambia, kasema, "Je! ulishikilia dini yako?"

¹⁴⁰ Nikasema, "La, ilinishikilia." Unaona? Unaona, nilikuwa na Yakini, kujua kwamba siku moja nitawaona tena. Amina. Nisingefaulu kama nisingalikuwa na hiyo Yakini. Iileta tofauti ndani yangu, mahali nilipofungiwa, kwa sababu nilijua kuwa nitawaona tena.

¹⁴¹ Sasa, kwa neema, nimefungwa Kwake Yeye aliyesema, "MIMI NIKO," si "Nilikuwa." "MIMI NIKO," daima, aliyepo daima, mwenye-, ajuaye yote, mwenye-, aliye na nguvu zote, asiye na kikomo, kwamba Yeye si "Nilikuwa." "MIMI NIKO," Yeye angali ni ufufuo. Yeye angali ni Nyota ya Kaskazini. Yeye angali ni kila kitu, kwangu mimi.

¹⁴² Musa alikuwa na yakini. Alipokutana na kile kichaka kilichowaka moto, hicho kilikuwa ni yakini kwake. Wakati Yoshua—wakati Yoshua...

¹⁴³ Loo, mnajua, wakati mwingine ukichukua yakini, yakini itakuongoza kwenye kitendawili. Hiyo ni kweli. Naam. Kitendawili ni kitu ambacho ni halisi, bali hakiwezi kuelezeka. Ni kitendawili.

¹⁴⁴ Wakati Yoshua akisimama pale, na akaona alikuwa na haja! Mungu alikuwa amemwagiza kuvuka kwenda huko na kuichukua ile nchi, awapige na kuwatoa hao watu wote, na—na kuweka Israeli katika nchi hiyo. Basi siku moja, majeshi yalishindwa, na huko nje nchini. Na ninii—na muda si muda wajua, alijua kuwa alikuwa amewashinda, mradi tu aliwafanya kutengana. Kwa hiyo, alipofanya hivyo, jua lilikuwa linaenda kutua. Naye Yoshua alikuwa amefungwa kwenye Yakini, Neno la Mungu, Muumba. Alifungwa kwenye kazi iliyomlazimu kufanya. Amina.

¹⁴⁵ Wakati mwingine haipendezi kuifanya; inakubidi kuumiza hisia, kukata na kukatakata. Bali ni yakini.

¹⁴⁶ Alikuwa na hitaji. Akasema, “Jua, simama kimya, huko! Mwezi, wewe ning’inia papo hapo!” Ndipo, kwa saa ishirini na nne, alisimama kimya. Loo, nena kuhusu kitendawili! Lakini alikuwa amefungwa kwenye yakini, akiwa na agizo. Naam, kweli, Mungu alikuwa amemwagiza.

Yohana alikuwa na hakika angeweza kuona Hua wakati alipokuja juu Yake.

¹⁴⁷ Wakati nilipoiona ile Nguzo ya Moto, kama Paulo njiani akienda Dameski, nilijua hiyo ilikuwa ni Yakini ya Mungu, kulikuwa kunakuja uamsho uliokuwa unaenda kuenea nchi mbalimbali. Nilijua Hiyo ingetangulia Kuja kwa pili kwa Yesu Kristo, nami ningali ninaiamini leo hii. Ndiyo Yakini yangu, ingawa ilikuwa ni kitendawili. Hakika, ilikuwa ni kitendawili, kwa Nguzo ya Moto kuning’inia huko juu angani. Na magazeti na kila kitu kupiga picha Yake.

¹⁴⁸ Ilikuwa ni kitendawili, siku ile nyingine, kwenye Machi tarehe 15, ama Mei tarehe 15, ninaamini...la, Machi tarehe 15, mwaka huu uliopita. Wakati, miezi mitatu au minne hapo kabla, *Mabwana, Ni Wakati Gani?*, kasema tungeenda huko nje, “Na Malaika saba wangekutana, na kurudi, na Ki—Kitabu cha Mihuri Saba kingefunguliwa.” Na nikisimama moja kwa moja pale na Ndugu Fred Sothmann, ambaye ndio kwanza tu aseme “amina” hapo, nikisimama pale karibu naye, mbona, niliwaambia, “Kutakuwapo kelele ambayo itaitikisa nchi.” Tena nikasema, “Itakuwepo. Ni BWANA ASEMA HIVI.” Iko kwenye kanda, kanda, kanda, kutoka Phoenix na kuzunguka kote. “Ni BWANA ASEMA HIVI.”

¹⁴⁹ Siku moja, nikisimama pale, nikiondoa magugu, ama maskini vichoma nguo kutoka kwa mguu wangu, kama ilivyokuwa; hapo ambapo Malaika saba walitokeza kutoka angani na kutikisa mahali hapo, mpaka, miamba, yenye uzito wa ratili hamsini au sitini, ikabingirika chini ubavuni mwa kilima. Hapo wakasimama Malaika saba wamesimama hapo, wakaniagiza kurudi ili kuleta Jumbe hizi, na kusema, “Moja kwa moja” wao “wangekutana na kueleza kilichofanyika.” Na ilifanyika hasa namna hiyo. Ndipo walipopaa Juu, namna *hiyo*, wakaenda maili thelathini juu hewani; na, katika siku iyo hiyo, walipiga picha Yake, sayansi ilipiga, na ikaenda kote ulimwenguni. Ni kitendawili, lakini ilikuwa ni Yakini. Ilinifunga kwa nguvu zaidi ndani ya Yesu Kristo, ikifunganisha maisha yangu ndani Yake. Ninajua ilionekana ya kigeni. Imekuwa daima.

¹⁵⁰ Ilikuwa ni kitendawili kwa Paulo, kukutana na Yesu katika barabara ya kuenda Dameski. Ni kitendawili wakati Mungu anapobadilisha moyo mweusi, wa mwenye dhambi na kuuosha mweupe katika Damu Yake Mwenyewe. Ni kitendawili. Hakika. Je! unaamini kitendawili? Nacho kitendawili hicho, kama ni kulingana na Neno la Mungu, kinaweza kuwa yakini yako. Kuongoka kwa Paulo kulikuwa ni kitendawili, na kikawa yakini yake.

¹⁵¹ Kumbukeni hapa, wakati fulani uliopita, nilikuwa nimeketi na maskini mwuza dawa, nasi tulikuwa tunazungumza katika mahali padogo. Akasema, “Ndugu Branham, ninataka kukuuliza jambo fulani.” Naye alikuwa ni Mbaptisti, mwenyewe. Akasema, “Je! unaamini kitendawili?”

Nikasema, “Hakika. Hakika naamini.”

¹⁵² Kasema, “Nisingelisimulia hili kwa mtu yeyote mwingine ila wewe,” kasema, “lakini ni—ninajua wewe unaamini hili.”

¹⁵³ Akasema, “Katika kipindi cha kudorora kwa uchumi,” kasema, “ilibidi wawe na hundi, kutoka kwa jimbo, ili kupata dawa kwa ajili ya mgonjwa.” Pia kasema, “Siku moja, nilikuwa nimeketi hapa nyuma katika duka la dawa.” Kasema, “Mwanangu alikuwa anawahudumia wateja.” Tena kasema, “Nilimwona m—mwanamke akiingia.” Kasema, “Alikuwa... Ungeweza kuona alikuwa anaenda kujifungua moja kwa moja.” Na kasema, “Maskini kitu hicho kilisimama kwa shida. Naye mume wake amevalia kifukara, wote wawili. Naye mke alijiegemeza ubavuni mwa kaunta. Naye mume alienda na kumwuliza mwanangu, akasema, ‘Ninalo agizo hapa kutoka kwa daktari.’ Akasema, ‘Hivi unaweza kunijazia na kuniruhusu nimpeleke mke wangu nyumbani?’ Akasema, ‘Nilijaribu kumfanya asimame kwenye huo mstari. Hebu angalia tu chini mtaani pale,’ akasema, ‘itakuwa ni saa nne au tano.’ Tena kasema, ‘Hawezi kusimama sasa, unaweza kuona.’”

154 Ndipo jamaa huyo mdogo akasema, “Bwana, si—siwezi kufanya hilo.” Akasema, “Itanibidi kupata hundi kwanza,” kasema, “maana si—siwezi kufanya hilo. Ni kinyume na sheria.” Pia kasema. . .

155 Baba yake akasema alikuwa ameketi huko nyuma akisikiliza, kuona kile mvulana huyo alisema. Ndipo akasema, “Hebu kidogo, mwanangu. Ni nini hiyo?”

156 Na akasema alitembea pale juu. Na yule mzee, Mkristo halisi, mzee mtakatifu kwelikweli. Alisema, “Ni kitu gani, ndugu yangu mpendwa?”

157 Ndipo akasema, “Bwana,” akasema, “Mimi. . .mke wangu, yuko karibu kabisa ku—ku—kujifungua.” Akasema, “Mi—mimi. . .ninalo agizo kutoka kwa daktari hapa; dawa fulani, lazima azipate sasa hivi.” Kisha kasema, “Ni—nilimpeleka huko chini kusimama chumbani kule.” Tena kasema, “Ni—ni. . . Angalia mlolongo huu,” kasema, “Nina shaka kama nitaweza kuingia ndani, alasiri ya leo.” Kasema, “Sijui tu kama—kama ungeweza kunijazia hili?” Kasema, “Nita—nitasimama kule chini; nita—nitakuletea pesa, hundi ambayo jimbo hulipa kwa ajili yake.”

158 “Mbona,” akasema, “hakika, bwana, nitakuletea.” Ndipo akaliweka tu chini agizo, akarudi nyuma. Alisema mvulana wake alirudi nyuma na kuanza kumhudumia mtu mwingine.

159 Kasema, “Maskini mama huyo aliangalia, mara mbili ama tatu. Amesimama tu pale, na jasho usoni mwake, alijua alikuwa mgonjwa sana. Naye ndugu huyo amesimama pale amemkumbatia, wajua, akisema, ‘Jikaze tu, mpenzi, sasa muda mfupi tu zaidi.’ Kasema, ‘Mwuza dawa mwema anaenda kutupatia dawa.’”

160 Akasema, “Nilitayarisha dawa upesi nilivyoweza, na kujaza agizo langu.” Ndipo kasema, “Nilipoanza kuiweka mkononi mwa mama huyo,” akasema, “Ndugu Branham, nilitazama na nilikuwa nikiiweka katika mkono wenye kovu la msumari.” Akasema, “Niliona miiba kwenye paji la uso Wake.” Akasema, “Nilifumba macho yangu, na kutazama nyuma.” Akasema, “Nilitambua pale pale, kadri nilivyokuwa nimemtendea ‘mdogo wa hawa watoto Wangu wadogo,’ alifanyiwa Yeye.”

161 Kasema, “Je! unasadiki hilo?”

Nikasema, “Kwa moyo wangu wote, daktari, ninaamini kila neno lake.”

162 Ni kitu gani? Akasema, “Tangu wakati huo, Kristo amekuwa wa zaidi kwangu. Kwa sababu, kufanya hivyo kwa ajili ya mwanamke huyo,” kasema, “ilikuwa ni kitendawili. Hapana shaka ila kwamba watu wa kawaida wasingaliadini hilo, bali,” kasema, “Niliwaza, nikuambie tu, kwa sababu ninajua umekuwa na matukio hayo.”

Nikasema, “Naam, bwana. Hiyo ni kweli,” nikasema.

¹⁶³ Ninakumbuka, wakati, Mtakatifu Martin, nikisoma juu yake. Wakati alipokuwa tu ni m—mvulana, aliitwa na Mungu. Watu wake walikuwa makafiri. Naye baba yake alikuwa—alikuwa kwa namna fulani, loo, sijui, nafikiri mwanajeshi, na—na ni sawa kwa wavulana wao kuwafuata. Alisema. . . siku moja akipitia mjini kule. Ninasahau mahali ilipokuwa sasa. Nami nafikiri alikuwa ni Mfaransa. Naye akasema alikuwa akipita kwenye pengo; palikuwa na mzee aliyekuwa amelala pale, akifa kwa baridi, hali ya baridi sana. Na watu walipita karibu, wasingempa chochote. Na kasema alisimama. Huku watu walikuwa wanakiri kabisa kuwa ni waaminio, nao wangepita, na kumwacha mzee huyo alale pale. Naye alikuwa anaombaomba apate kitu cha kujifunika, kasema alikuwa anakufa kwa baridi.

¹⁶⁴ Basi Mtakatifu Martin anaenda pale, kabla ya kuongoka kwake, sasa, akachukua koti lake mwenyewe, akiwa ni mwanajeshi, na kulikata nusu vipande viwili na kumfunika huyo mzee ombaomba katika hicho, na kujifunika kile kingine. Watu walimcheka, kasema, “Mwanajeshi anayeonekana wa kuchekesha, huku amevaa nusu ya koti.” Unaona, inakufanya kutenda mambo yasiyo kawaida. Kulikuwa na kitu ndani yake, kwamba aliamini kuwa kulikuwa na Mungu.

¹⁶⁵ Usiku huo, baada ya kumaliza zamu na kulala kidogo, akaamka. Mtu fulani alimwamsha, ndipo akatazama. Akisimama kando ya kitanda chake, na hapo alisimama Yesu amefunikwa kile kipande kingine cha koti. Huo ulikuwa ndio mwanzo wa Mtakatifu Martin.

¹⁶⁶ Ilikuwa ni nini? Alikuwa na yakini, kwamba Neno la Mungu ni kweli. “Kile unachowafanyia hawa wadogo Wangu, umenifanyia Mimi.” Ndugu, nimefungwa kwenye hiyo Yakini. Nami ninajua kwamba kila mmoja wenu. . .

¹⁶⁷ Badala ya kuwa na wito wa madhabahuni, asubuhi ya leo, nafikiri ningependa kuwa na wito wa kujiweka wakfu. Hebu tujiweke wakfu kwa hii Yakini. Je! mnaamini kwamba Neno ni yakini ya Mungu? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Je! mnaamini kwamba Yeye ni yule yule leo ambaye alikuwa daima? [“Amina.”]

¹⁶⁸ Wapo wahudumu humu ndani, hivi hamngependa kuyaweka wakfu maisha yenu, tu, mchukue tu Yakini? Tunataka nini leo? Tunataka nini na kadi ya ushirika au stakabadhi? Tunataka Yesu Kristo. Hatujafungwa kwenye kadi ya ushirika. Tumefungwa kwenye Neno la Mungu, “Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele.” Je! mnaamini hilo? [Wahudumu wanasema, “Amina.”—Mh.]

¹⁶⁹ Hebu tusimame tu kwa miguu yetu sasa na tuyaweke wakfu maisha yetu. Ninataka yangu, pia. Ninajifunga mwenyewe, upya. Ninachunguza kifungo changu, kifungo kimefungwa.

Ninachunguza yakini yangu. “Bwana, iwapo kuna kitu chochote ndani yangu, kando na Neno Lako, kiondoe. Sijui chochote kingine ila Wewe. Sitaki kujua chochote kingine ila Wewe.” Sasa, kila mmoja, kwa njia yako mwenyewe.

¹⁷⁰ Nimekuwa nikizungumza nanyi kote katika juma. Nimewaambieni Kweli. Mungu ameithibitisha Kweli. Ameifanya tena na tena, na tena mara nyingine. Mnajua kilicho Yakini. Sasa kwangu mimi na wewe, pamoja, enyi wanawake wote, enyi wanaume wote, wavulana, wasichana, chochote ulicho, hebu tuninii; enyi nyote wanakwaya, enyi—enyi watu wote hapa juu, kila mahali, pamoja; chini katika orofa ya chini, juu kwenye roshani, kote kwenye kuta, nyuma pembeni; popote tulipo, hebu tumchukue Yesu, Yakini yetu, kwa kuwa hatuna budi kuja kwenye mabonde ya kivuli cha mauti. Sijui chochote kingine ila Yeye. Yeye ndiye Yakini yangu, kwa sababu Yeye amefufuka katika maisha yangu nami ninajua Yeye ni halisi.

¹⁷¹ Hebu tuinue tu mikono yetu sasa na kuomba. Hebu tufanye ibada yetu ya kujiweka wakfu.

¹⁷² Bwana Yesu, Neno Lako ni tangu zamani, Ndilo mwanzo tena mwisho. Mimi sasa, pamoja na kusanyiko hili, ninajiweka wakfu, upya, juu ya mimbara hii leo. Ninaombea kanisa hili, Maskani ya Life, kwa ajili ya kujiweka wakfu. Tatua tofauti zote, jalia zote zitoweke, zilizopita ziwe zilizopita. Wahudumu wa Injili, ambao wana wasiwasi...na kuwazia jambo fulani lingetendeka. Ee Mungu, tunajifunga wenyewe, asubuhi ya leo, kwa Yesu Kristo Neno; na kuazimu kutojua chochote kingine ila Kristo, na Yeye amesulubiwa. Ee Nyota ya Kaskazini, Ee Roho Mtakatifu, Ee Dira ya Mungu, njoo sasa ndani ya kila moyo. Nasi tunajiweka wakfu Kwako, kupitia Jina la Yesu Kristo. Utukufu kwa Mungu! Amina.

Vema, ndugu.



YAKINI SWA63-1201M
(An Absolute)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumapili asubuhi, tarehe 1 Desemba, 1963, katika Maskani ya Life kule Shreveport, Louisiana, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2019 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org